**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

**KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**

# MAONI YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA WA FEDHA 2018/19 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/20

OFISI YA BUNGE
**DODOMA**

**03 JUNI, 2019**

## 1.0 UTANGULIZI.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2018/19, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/20 ambayo inajumuisha Mafungu Saba (7)ambayo ni Fungu 07 - Ofisi ya Msajili wa Hazina, Fungu 10 - Tume ya Pamoja ya Fedha, Fungu 13 - Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu, Fungu 21- Hazina, Fungu 22 - Deni la Taifa, Fungu 23 - Mhasibu Mkuu wa Serikali, Fungu 50 - Wizara ya Fedha na Mipango. Taarifa hii itajumuisha pia Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** moja ya jukumu la Kamati ya Bunge ya Bajeti kama yalivyoainishwa kwenye Nyongeza ya Nane kifungu cha 9 cha Kanuni za kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 ni pamoja na kusimamia shughuli za Wizara ya Fedha na Mipango na taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo. Aidha, kifungu cha 9 (1) (c) cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 pia kinaipa Kamati jukumu la kupitia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu – 45, Mfuko wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali. Kwa muktadha huo, katika nyakati tofauti, Kamati ilikutana na kufanya mashauriano na Serikali na hatimaye kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango na Mafungu yake pamoja Fungu 45 - Mfuko wa Ofisi ya Taifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango yameorodheshwa kwenye Tangazo la Serikali Na. 144 la terehe 22 Aprili, 2016. Pamoja na mambo mengine Wizara ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa sera za mapato na matumizi ya umma pamoja na kusimamia sera za fedha na

uchumi kwa ujumla. Majukumu hayo yanatekelezwa kupitia mafungu yaliyo chini yake kama ifuatavyo: -

i. Fungu 07 - Ofisi ya Msajili wa Hazina imepewa jukumu la kusimamia na kulinda rasilimali zilizowekezwa na Serikali katika Mashirika na Taasisi za Umma na majukumu mengine kama yalivyoainishwa kwenye Sheria ya Msajili wa Hazina Sura Na. 370.
ii. Fungu 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha ni Asasi ya Muungano wa Tanzania iliyoundwa kwa mujibu wa Ibara 134 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na kuanzishwa kwa Sheria ya Tume ya Pamoja ya Fedha ya mwaka 1996, Sura 140. Jukumu kuu la Tume ni kuwa chombo cha ushauri kuhusiana na mambo yote ya Muungano yanayohusu fedha baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na majukumu mengine kama yalivyoainishwa kwenye Ibara ya 134(2) ya Katiba.
iii. Fungu 13 – Kitengo cha kudhibiti Fedha Haramu; Kitengo hichi ni chombo cha kiinteligensia kilichoanzishwa chini ya Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu ya Mwaka 2006, Sura Na. 463 mahsusi kwa ajili ya kupambana na utakatishaji wa fedha haramu pamoja na ufadhili wa vitendo vya ugaidi nchini.
iv. Fungu 21- Hazina; Ofisi hii ina majukumu makuu matatu. Jukumu la kwanza ni kusimamia ukusanyaji wa mapato na matumizi ya fedha za Serikali, Pili ni kusimamia utekelezaji wa bajeti ya Serikali na Tatu ni kuhakikisha kunakuwa na kudhibiti Deni la Taifa ili liendelee kuwa himilivu.
v. Fungu 22 – Deni la Taifa; Idara hii inajukumu kubwa la kulipa madeni ya ndani na nje ya nchi (Principal debt) pamoja na riba (Interest). Aidha Idara hii pia inajishughulisha na mafao ya pensheni kwa wastaafu pamoja na michango ya mwajiri.
vi. Fungu 23- Mhasibu Mkuu wa Serikali; Idara hii ina jukumu la kusimamia matumizi ya fedha za Serikali na kutoa miogozo ya mifumo ya kifedha inayopaswa kutumiwa na taasisi zote za umma.

vii. Fungu 50 -Wizara ya Fedha na Mipango inajukumu la msingi la kusimamia uchumi jumla kupitia sera za fedha (Fiscal Policy) na matumizi na mifumo ya kifedha kwa ajili ya kuimarisha ukuaji wa uchumi (Monetary Policy).

## 2.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA MAJUKUMU YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA WA FEDHA 2018/19

### 2.1. Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa Fedha 2018/19, Wizara ya Fedha na Mipango iliidhinishiwa na Bunge kutumia jumla ya **shilingi 12,058,714,013,500** kwa mafungu yote saba (7) . Kati ya fedha hizo **Shilingi 10,763,501,474,000** zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambayo yanajumuisha malipo ya deni la Serikali (pamoja na riba) na **Shilingi 1,295,212,539,500** zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Aidha, Kamati ilipitia Bajeti ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ambapo kiasi cha **shilingi 69,106,308,000** kiliidhinishwa kwa matumizi ya Ofisi hii katika mwaka 2018/19. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 55,394,216,000** zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 13,712,092,000** zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya maaendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Aprili, 2019 jumla ya **shilingi 8,253,791,005,658** zilikuwa zimetolewa kwa Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na mafungu yake yote hii ikiwa ni sawa na **asilimia 68.4** ya Bajeti yote ya Wizara kwa kipindi husika. Kati ya fedha hizo **Shilingi 8,233,112,879,443** sawa na **asilimia 76.5** ya lengo zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 20,678,126,214** zilikuwa ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo sawa na **asilimia 1.6** tu ya Bajeti.

Aidha, kwa upande wa Fungu 45 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali**,** lilitengewa jumla **ya shilingi 57,735,146,884** kwa ajili ya matumizi ya

kawaida na maendeleo. hadi kufikia mwezi April, 2019 lilikuwa limepokea kiasi cha **shilingi 41,736,336,731** sawa na **asilimia 75.3** Kati ya fedha hizo **shilingi 41,536,336,731** zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 1,602,930,884** zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo ambayo ni sawa na **asilimia 11.7** ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge.

Aidha, **Jedwali Na. 1** hapo chini linaonyesha mgawanyo wa bajeti kwa kila fungu pamoja na utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha robo tatu ya mwaka wa fedha 2018/19.

**Mheshimiwa Spika**, Kama ambavyo jedwali linaonyesha, Utekelezaji wa bajeti ya Mafungu ya Wizara ya Fedha na Mipango umekuwa si wakuridhisha hasa kwa upande wa Bajeti ya maendeleo. Katika mafungu yote matano yanayopokea fedha za maendeleo ni fungu moja tu **(Fungu-50)** ambalo limepokea fedha za maendeleo zaidi ya asilimia 50

**Jedwali Namba 1. Utekelezaji wa Bajeti Kwa Mafungu ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2018/19**

| FUNGU | JINA LA FUNGU | BAJETI ILIYOIDHINISHWA 2018/19 | | FEDHA ILIYOTOLEWA HADI APRILI, 2019 | | ASILMIA YA FEDHA ZILIZOTOLEWA HADI APRILI, 2019 | | ASILIMIA KIASI CHOTE KILICHOTOLEWA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Matumizi ya kawaida | Maendeleo | Matumizi ya Kawaida | Maendeleo | Matumizi ya Kawaida | Maendeleo | (%) |
| 07 | Msajili wa Hazina | 54,592,065,000 | 1,650,000,000 | 15,771,612,109 | 649,895,000 | 28.9 | 39.4 | 29.2 |
| 10 | Tume ya Pamoja ya Fedha | 2,155,075,000 | - | 1,440,202,822 | - | 66.8 | 0 | 66.8 |
| 13 | Kitengo cha Udhibiti Fedha Haramu | 2,015,586,000 | 248,363,000 | 1,575,970,211 | 0 | 78.2 | 0.00 | 69.6 |
| 21 | Hazina | 531,890,056,000 | 1,247,611,267,500 | 352,032,558,607 | 11,659,660,085 | 66.2 | 0.93 | 20.4 |
| 22 | Deni la Taifa | 10,013,706,140,000 | - | 7,734,740,415,117 | - | 77.2 | 0 | 77.2 |
| 23 | Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali | 46,725,409,000 | 3,200,000,000 | 40,155,147,427 | 2,726,434,843 | 85.9 | 85.2 | 85.9 |
| 50 | Wizara ya Fedha na Mipango | 57,022,927,000 | 28,790,817,000 | 27,851,947,727 | 3,301,205,402 | 48.8 | 11.5 | 36.3 |
| JUMLA | | | | | | | | |
| 45 | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu ya Serikali | 55,394,216,000 | 13,712,092,000 | 41,736,336,731 | 2,340,930,884 | 75.3 | 17.0 | 63.8 |

**Jedwali Namba 2. Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo Kwa Mafungu ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2018/19**

| FUNGU | JINA LA FUNGU | BAJETI YA MAENDELEO ILIYOIDHINISHWA 2018/19 | | FEDHA ILIYOTOLEWA HADI APRILI, 2019 | | ASILMIA YA FEDHA ZILIZOTOLEWA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Ndani | Nje | Ndani | Nje | Ndani | Nje |
| 07 | Msajili wa Hazina | 1,000,000,000 | 650,000,000 | 0 | 649,895,000 | 0 | 99.9 |
| 10 | Tume ya Pamoja ya Fedha | - | - | - | - | - | |
| 13 | Kitengo cha Udhibiti Fedha Haramu | - | 248,363,000 | - | 0 | 0 | |
| 21 | Hazina | 1,236,190,593,500 | 11,420,674,000 | 10,950,000,000 | 709,660,085 | 0.89 | 6.2 |
| 22 | Deni la Taifa | - | - | | | | |
| 23 | Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali | 2,000,000,000 | 1,200,000,000 | 1,620,641,093 | 1,105,793,750 | 81.0 | 92.1 |
| 50 | Wizara ya Fedha na Mipango | 19,642,535,000 | 9,148,282,000 | 1,276,831,402 | 2,024,374,000 | 6.5 | 22.1 |
| JUMLA | | | | | | | |
| 45 | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu ya Serikali | 7,200,000,000 | 6,512,092,000 | 1,520,535,884 | 820,395,000 | 21.1 | 12.6 |

## 2.2. Uchambuzi wa Kamati kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa mafungu ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2018/19.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati katika mafungu haya ulibaini kuwa :-

i. Mafungu **matano 5** (Fungu 13- Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu, Fungu 22- Deni la Taifa, Fungu 23- Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, Fungu 45- Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali na Fungu 50- Wizara ya Fedha na Mipango) yalipokea zaidi ya asilimia 60 ya fedha za matumizi ya kawaida zilizoidhinishwa na Bunge; na
ii. Mafungu **mawili 2** (Fungu 10- Tume ya Pamoja ya Fedha na Fungu 21- Hazina) yalipokea zaidi ya asilimia 50 na Fungu moja, (Fungu 07 Msajili wa Hazina) lilipokea asilimia 20 tu ya bajeti nzima ya fedha za matumizi ya kawaida.

**Mheshimiwa Spika,** kati ya **Shilingi 1,295,212,539,500** zilizoidhishwa na Bunge kwa Wizara kwa mwaka wa fedha 2019/20 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ni **20,678,126,214** sawa na **asilimia 1.6** ndiyo zimetolewa**.** Aidha, ni fungu moja tu, Fungu 23- Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali ndilo lilopata zaidi ya **asilimia 50** ya bajeti ya maendeleo kama iliyoidhinishwa na Bunge. Aidha, kati ya fedha zote, fedha za ndani ndizo zilizotolewa kwa kiasi kikubwa ikilinganishwa na fedha za nje. Hivyo, utekelezaji huu hafifu wa bajeti za mafungu ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na kutopatikana kwa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo kutoka nje.

**Mheshimiwa Spika,** mwenendo huu wa utolewaji wa fedha usioridhisha unaathiri utekelezaji wa majukumu ya Msingi ya Wizara.

#### 2.1.1. Fungu 07 - Ofisi ya Msajili wa Hazina

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2018/19, Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya **shilingi 56,242,065,000** hata hivyo hadi kufika mwezi Aprili, 2019 kiasi cha **shilingi 16,421,507,109** ndicho kilikuwa kimetolewa na Hazina ikiwa ni sawa na asilimia **29.1** ya lengo.

**Mheshimiwa Spika,** utolewaji wa fedha kwa fungu hili umekuwa ni chini ya asilimia 50 katika kipindi husika kwa miaka mitatu mfululizo. Katika kipindi kama hiki kwa mwaka wa fedha 2017/18 na 2016/17 Ofisi ilipokea bajeti kati ya asilimia **asilimia 7.7** hadi **17.25** ya fedha yote iliyoidhinishwa na Bunge. Mwenendo huu si wa kuridhisha hata kidogo ukizingatia umuhimu wa majukumu ya Ofisi ya Msajili wa Hazina. Aidha, katika mafungu yote 7, ya Wizara ya fedha na Mipango Fungu 07 ndio fungu pekee ambalo limekuwa linapokea fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida chini ya **asilimia 30.**

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa mwaka wa fedha 2018/19 ilitenga **shilingi 45,000,000,000** fedha kwa ajili ya matumizi maalum yanayojumuisha kulipa madeni ya mashirika ya umma na kurekebisha mashirika yenye matatizo ya kimtaji. Hadi kufikia mwezi Machi, 2019 zilikuwa zimetolewa **shilingi 6,300,000,000** tu sawa na **asilimia 14** sawa. Hii ikiashiria kwamba Serikali bado haijatekeleza kwa vitendo nia yake ya kuwekeza kwenye mashirika ya umma ili yaweze kutoa mchango mkubwa zaidi katika Maendeleo ya Taifa.

#### 2.1.2. Fungu 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Machi, 2019, Tume ilikuwa imepokea kiasi cha **shilingi 1,440,202,822** kati ya **shilingi 2,155,075,000** zilizoidhinishwa ikiwa ni sawa na **asilimia 66.8** ya bajeti yote. Kamati inasisitiza ukamilishaji wa haraka wa mchakato wa mapitio ya mapendekezo ya mwongozo wa uendeshaji na usimamizi wa Akaunti ya Fedha ya Pamoja (AFP) na hatimaye kufunguliwa kwa akaunti

hiyo. Suala hili ni la muda mrefu tangia kuanza kwa chombo hiki mwaka 2003 lakini bado utekelezaji haujafanyika ipasavyo.

### 2.1.3. Fungu 13 – Kitengo cha kudhibiti Fedha Haramu

**Mheshimiwa Spika,** hadi mwezi Aprili, 2019 Kitengo kilikuwa kimepokea kiasi cha **shilingi 1,575,970,211** fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikiwa ni sawa na **asilimia 69.6** Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo, Kitengo kilitengewa kutumia kiasi cha **shilingi 248,363,000** lakini hadi Aprili, 2019 hamna fedha zozote zilizotolewa na hivyo kufanya bajeti ya maendeleo kutotekelezwa.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na utolewaji wa fedha unaoridhisha kwa upande wa fedha za matumizi ya kawaida, bado kitengo hiki hakijaweza kufanya kazi iliyokusudiwa kwa ufanisi kutokana na changamoto zifuatazo;

i. Kitengo kufanya kazi kwa kutegemea watumishi wa kuazima kutoka Idara nyingine za Serikali na
ii. Kitengo kutegemea taarifa kutoka vyombo vingine pamoja na uwezo wa kimfumo wa kitengo kugundua na kudhibiti miamala shuku.

Hivyo kamati inaishauri Serikali kushughulikia haraka changamoto hizo ili kitengo kiweze kufanya kazi kwa ufanisi ikiwemo kutoa fedha za miradi ya maendeleo.

### 2.1.4. Fungu 21- Hazina

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Aprili, 2019 fungu hili lilikuwa limepokea **shilingi 1,599,643,826,107** kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na **asilimia 20.4** ya bajeti nzima ya fedha za matumizi ya kawaida. Aidha, kwa fedha za maendeleo fungu lilikuwa limepokea **shilingi 11,659,660,085** fedha za maendeleo sawa na **asilimia 0.93**

Aidha, bajeti nzima ya Fungu 21 katika kipindi hicho ilikuwa imetolewa kwa **asilimia 20.4** tu.

**Mheshimiwa Spika,** Fungu hili pamoja na majukumu mengine ndilo hasa linasimamia sera ya fedha na sera za kibajeti. Aidha, kwa kiasi kikubwa fungu hili linahusika moja kwa moja na mikakati ya kupunguza umasikini na kukuza uchumi. Hivyo, utolewaji wa fedha za maendeleo kwa **asilimia 0.93** tu ni kuathiri juhudi za Serikali ambazo kimsingi zina nia ya kutokomeza umasikini na kukuza uchumi.

### 2.1.5. Fungu 22 – Deni la Taifa na Huduma Nyingine

**Mheshimiwa Spika,** Malipo ya deni la Serikali ambayo ni mtaji pamoja na riba yameongezeka kutoka **Shilingi trilioni 7,817,118,000,000** mwaka 2017/18 hadi **Shilingi trilioni 8,372,951,000,000** mwaka 2018/19 sawa na ongezeko la **asilimia 7.11.**

**Mheshimiwa Spika,** Tathimini ya uhimilivu wa deni la taifa iliyofanyika mwezi Desemba 2018 na matokeo ya awali yanaonesha kuwa deni ni himilivu kwa muda mfupi, wa kati na mrefu. Takwimu zinaonyesha kwa wastani katika kipindi cha miaka 3 Serikali hutenga **shilingi 8,017,549,000,000** kwa mwaka kwa ajili ya kugharamia deni la taifa. Hivyo, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuendelea kutafuta vyanzo vingine vya mikopo ya masharti nafuu ili kugharamia miradi ya maendeleo.

**Jedwali Namba 3: Malipo ya Deni la Serikali**

| Na. | | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ndani | 5,973,775,000,000 | 6,013,631,000,000 | 4,899,168,000,000 |
| 2. | Nje | 1,903,343,000,000 | 2,359,320,000,000 | 2,963,410,000,000 |
| 3. | **Jumla** | **7,817,118,000,000** | **8,372,951,000,000** | **7,862,578,000,000** |

### 2.1.6. Fungu 23- Mhasibu Mkuu wa Serikali

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Aprili, 2019 Idara hii ilikuwa imepokea jumla ya **shilingi 42,881,582,270** sawa na **asilimia 82.9** ya bajeti yote iliyoidhinishwa na Bunge. Fungu hili, ni fungu pekee la Wizara ya Fedha na Mipango ambalo limepokea fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa **asilimia 85.2** ya fedha zote za maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Idara hii kwa kuweza kusimamia mfumo wa udhibiti wa matumizi ya fedha za umma ikiwa ni pamoja na uanzishwaji wa Akaunti Jumuifu ya Hazina (TSA). Aidha, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, utekelezaji wake bado unaathiriwa na upatikanaji wa mtandao wa uhakika hivyo unaathiri pia mifumo mingine ya malipo hasa katika ngazi za chini za Halmashauri. Hivyo, Serikali itafute namna ya kuondokana na changamoto hii ili mfumo uweze kufanya kazi kwa ufanisi Zaidi.

### 2.1.7. Fungu 50 -Wizara ya Fedha na Mipango

**Mheshimiwa Spika**, Fungu 50 – Wizara ya Fedha na Mipango katika mwaka wa fedha 2018/19 liliidhinishiwa jumla ya **shilingi 85,813,744,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Aprilii, 2019 Wizara ilikua imepokea jumla ya **shilingi 31,153,153,129** sawa na **asilimia 36.3** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo **shilingi 20,393,917,182** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, **shilingi 5,479,287, 356** kwa ajili ya mishahara na **shilingi 3,301,205,402** kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa Idara na Taasisi zilizo chini ya fungu hili.

**Mheshimiwa Spika,** ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kuna umuhimu wa Serikali kuhakikisha kuwa Wizara hii inapelekewa fedha zake kama zilivyoidhinishwa na Bunge. Kushindwa kufikiwa kwa malengo ya Wizara kutapelekea kushindwa kufikiwa kwa malengo ya nchi hasa kwa upande wa ukuaji wa uchumi.

### 2.1.8. Fungu 45 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Bajeti ilikutana na Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili kufanya mashauriano kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu hili.

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ni taasisi yenye jukumu la kufanya ukaguzi wa mapato na matumizi ya Serikali, kama yalivyoidhinishwa na Bunge. Kwa mujibu wa Hati ya Majukumu ya mwaka 2018, Ofisi imepewa majukumu yafuatayo:

i. Kukagua hesabu za Wizara, Mikoa, Halmshauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji, Ofisi za Balozi za Tanzania zilizoko nje ya nchi, Wakala za Serikali, Mashirika ya Umma, pamoja na Miradi ya Maendeleo inayogharamiwa na wafadhili na kutoa taarifa ya ukaguzi huo Bungeni juu ya mapato na matumizi ya fedha za Umma;
ii. Kujenga, kukuza na kuimarisha utamaduni wa uwajibikaji katika Wizara na Taasisi za Serikali, Mikoa na Halmshauri;
iii. Kuhakikisha kwamba, inajiridhisha kuwa upo uwajibikaji wa kutosha katika kusimamia na kudhibiti ipasayo ukusanyaji wa mapato na matumizi ya Serikali; na
iv. Kuhakikisha kuwa jamii ya Tanzania inapata faida au tija kutokana na matumizi bora ya fedha za Umma, na mali za Umma zinahifadhiwa, kutunzwa na kulindwa ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2018/19 Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali iliidhinishiwa jumla ya kiasi cha **Shilingi 62,878,658,000** kutoka Mfuko Mkuu kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo mishahara ni **Shilingi 16,647,699,000** matumizi mengineyo (OC) **Shilingi 32,518,867,000** na **Shilingi 13,712,092,000** zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo fedha za ndani zilikuwa **shilingi 7,200,000,000** na **shilingi 6,512,092,000** ni fedha za nje. Kwa upande wa maduhuli, Ofisi ilikadiriwa kukusanya kiasi cha **shilingi 6,227,650,000.** Maduhuli ya Ofisi hii yanatokana na marejesho ya gharama za ukaguzi (reimbursable costs) wa Mashirika ya Umma, ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo inayosimamiwa na Wizara chini ya Divisheni ya Serikali Kuu pamoja na ile ya miradi chini ya Divisheni ya Hesabu za Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza Bajeti hiyo hadi kufikia mwezi Aprilii, 2019 Ofisi ilikuwa imepokea jumla ya kiasi cha **shilingi 44,077,267,615** kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali. Kiasi hicho ni sawa na **asilimia 54.05**. Kati ya kiasi hicho, **shilingi 16,647,699,000** ni kwa ajili ya mishahara, **Shilingi 30,789,493,681** ni kwa Matumizi ya kawaida na shilingi **shilingi 2,340,930,884** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo**.**

**Mheshimiwa Spika,** kiasi hicho cha bajeti kilichotolewa kimeiwezesha Ofisi kutekeleza shughuli mbalimbali zilizokuwa zimepangwa kulingana na fedha zilizopokelewa kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na makusanyo ya ndani. Aidha, mwenendo wa utolewaji wa fedha kutoka Mfuko Mkuu kwa Ofisi kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo umebaki kuwa wa changamoto ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2019 kiasi kilichokuwa kimepokelewa ni **asilimia 54** tu ya lengo la mwaka.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya tathmini ya mwenendo wa sura ya bajeti ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi za Hesabu za Serikali iliyokuwa inatengewa na Serikali kwa kipindi cha miaka 3 kuanzia 2017/18 hadi

2019/20 na ilibaini kuwa bajeti ya Ofisi imekuwa ikishuka mwaka hadi mwaka na hivyo kuifanya Ofisi kutofikia malengo yake ya kiukaguzi inayokuwa imejiwekea na hatimaye kushindwa kuendana na viwango vya kimataifa vilivyowekwa kwa uhuru wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kutolewa kwa kiwango cha chini cha bajeti kwa Ofisi hii kumepelekea Ofisi hii kushindwa kufanya ukaguzi katika maeneo mengi zaidi yaliyokuwa na umuhimu wa kufanyiwa ukaguzi.

**Mheshimiwa Spika,** ufinyu huo wa bajeti umeisababisha Ofisi kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Baadhi ya shughuli zilizoshindwa kutekelezwa ni zifuatazo: -

i. Ofisi imeshindwa kupanua mawanda ya ukaguzi kufikia maeneo ambayo Ofisi inaona yana viashiria vya mwenendo wenye shaka katika mapato na matumizi ya fedha za Serikali;
ii. Ofisi imeshindwa kufanya uhakiki wa kina hasa utekelezaji wa mapendekezo yanayotolewa kwa Halmsahuri kupitia taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi yanayotolewa kwa Halmashauri kupitia taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Fedha nyingi za Umma zinaelekezwa katika Halmshauri, ni muhimu Ofisi ya CAG ikawezeshwa ili kufanya ufuatiliaji wa karibu wa utekelezaji wa mapemdekezo yanayotolewa kwa Halmshauri husika;
iii. Ofisi imeshindwa kukamilisha ujenzi wa majengo ya Ofisi katika mikoa iliyolengwa kutokana na kutopata fedha za maendelo kama zinavyoidhinishwa;
iv. Ofisi imeshindwa kuendana na viwango vya kimataifa vilivyowekwa kwa uhuru wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikalu (ISSAI 10); na

v. Ofisi imeshindwa kuwajengea uwezo wakaguzi kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vya ukaguzi na katika maeneo mapya ya kipaumbele ya kikaguzi.

## 3.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO PAMOJA NA OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/20.

### 3.1 Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mafungu 7 ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2019/20.

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2019/20 imekadiriwa kutumia jumla ya **Shilingi 11,286,170,133,820** kwa mafungu yote Saba (7). Kati ya fedha hizo, **Shilingi 10,604,033,118,820** ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo (OC) na kwa ajili ya kulipia Deni la Serikali na huduma nyingine, **shilingi 608,371,517,988** ajili ya mishahara na **Shilingi 730,581,941,731** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo inayotarajiwa kutekelezwa na Wizara katika kipindi husika.

### 3.2 Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali (NAOT) kwa Mwaka wa Fedha 2019/20.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Bajeti ilikutana na Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili kujadiliana na kufanya mashauriano kuhusu nyongeza ya **Shilingi bilioni 3, 5000,000,000** iliyokuwa ikiombwa baada ya kupewa ukomo wa Bajeti. Fedha hizo zinazohitajika kwa ajili ya kaguzi maalum nje ya zile zinazopangwa na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ambapo maombi hupokelewa kutoka Taasisi mbalimbali za Serikali, kaguzi maalum kwa Halmshauri zilizopata hati chafu

pamoja na kaguzi za mamlaka 13 za maji ambazo hazina uwezo wa kugharamia kaguzi zake. Kukosekana kwa nyongeza hiyo ya fedha kutaathiri utendaji kazi wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi katika mwaka wa fedha 2019/20. Baada ya majadiliano Serikali iliridhia kuongeza fedha hizo kwa ofisi ya **NAOT** pindi mahitaji hayo yatakapojitokeza.

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi kwa mwaka wa fedha 2019/20 imelenga kuimarisha ukaguzi wa mapato na matumizi ya Serikali kuimarisha uwajibikaji na uwazi kwenye matumizi ya rasilimali za umma ambapo ilipanga kutumia **shilingi 64,917,248,417** kulingana na vipaumbele na kazi za Ofisi zilizolengwa kutekelezwa. Aidha, kwa mujibu wa ukomo uliotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango, Fungu 45 limetengewa jumla ya **shilingi 61,376,878,000**. Kati ya fedha hizo, **shilingi 14,084,139,000** ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi, **shilingi 34,305,459,417** ni fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali, **shilingi 6,227,650,000** ni fedha kutoka ukaguzi wa Wakala/Taasisi na Mashirika ya Umma na **shilingi 6,300,000,000** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo ambazo **shilingi 5,000,000,000** ni fedha za ndani na **shilingi 1,300,000,000** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati bado inasisitiza umuhimu wa kuhakikisha Fungu 45 linapatiwa rasilimali fedha za kutosha zinazoendana na vipaumbele, kazi na mahitaji halisi ya Ofisi ili iweze kutekeleza majukumu yake ya kikatiba. Aidha, ni maoni ya Kamati kuwa maombi yote ya kaguzi kutoka taasisi na wizara za Serikali zipitie kwanza Hazina ili kuwezesha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kufanya kaguzi hizo na sio maombi hayo kupelekwa moja kwa moja kwa Mkaguzi Mkuu.

**Jedwali Namba 4. Maombi ya Fedha Kwa Wizara ya Fedha na Mipango na Mafungu yaliyo Chini Wizara Pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa Mwaka 2019/20.**

| FUNGU | MATUMIZI MENGINEYO (OC) | MISHAHARA | MIRADI YA MAENDELEO | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| **07** | 37,229,786,000 | 3,281,016,000 | 2,300,000,000 | 42,810,802,000 |
| **10** | 1,558,142,000 | 649,793,000 | - | 2,207,935,000 |
| **13** | 2,015,586,000 | - | 200,295,998 | 2,215,881,998 |
| **21** | 736,280,618,000 | 536,520,631,988 | 683,717,888,733 | 1,956,519,138,721 |
| **22** | 9,721,127,000,000 | 8,885,708,000 | - | 9,730,012,708,000 |
| **23** | 37,036,734,000 | 7,029,314,000 | 3,300,000,000 | 47,366,048,000 |
| **50** | 27,792,514,000 | 37,920,916,000 | 34,763,757,000 | 100,477,187,000 |
| **JUMLA** | **10,563,040,380,000** | **594,287,378,988** | **724,281,941,731** | **11,881,609,700,717** |
| **45** | 40,992,739,000 | 14,084,139,000 | 6,300,000,000 | 61,376,878,000 |
| **JUMLA KUU** | **10,604,033,119,000** | **608,371,517,988** | **730,581,941,731** | **11,942,986,578,719** |

## 4.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI

**Mheshimiwa Spika,** baada ya Kamati kupitia utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2018/19 pamoja na mapato na matumizi ya mafungu husika kwa mwaka wa fedha 2019/20; Kamati inapenda kutoa maoni na mapendekezo yake kama ifuatavyo: -

### 4.1 Mamlaka ya Waziri wa Fedha katika masuala yote ya Fedha

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango na Taasisi zake katika kusimamia Sera za Fedha na Sera za Kiuhasibu (Monetary and Fiscal Policies) na kuwa ndiye msimamizi mkuu wa masuala yanayohusu fedha. Hata hivyo, hivi karibuni kumeibuka utaratibu kwa baadhi ya Wizara na mamlaka

ya Mikoa na Wilaya kutoheshimu mamlaka haya ya Wizara ya fedha na Mipango na hivyo kutoishirikisha Wizara (*Consultation*) katika uanzishwaji/uwekaji wa tozo, ushuru na ada katika sekta zao. Jambo hili limepelekea baadhi ya tozo, ada na ushuru unaoanzishwa kuwa kero kwa wananchi na wafanyabiashara.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Wizara ya Fedha na Mipango ndiyo yenye *Instrument* ya kusimamia masuala yote ya fedha na taratibu zake ni vema kukafanyika *harmonization* ya Sheria zote ili kuzitaka Wizara na mamlaka nyingine zote kulazimika kukubaliana na Wizara ya Fedha na Mipango kabla ya kuanzisha tozo, ada au ushuru wa aina yoyote.

### 4.2 Utaratibu wa Kubakiza kiasi cha mapato (*Retention)*

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa mapitio wa bajeti ya Fungu 50 - Wizara ya Fedha na Mipango, Kamati ilibaini kuwa kuna baadhi ya taasisi zilizo chini ya Wizara ya Fedha na mipango ambazo zinapokea mishahara kutoka Serikali kuu bado zinatumia utaratibu wa *retention*. Taasisi hizo ni pamoja na Taasisi za Mafunzo IFM, IAA, TIA; Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi (NBAA), Wakala wa Ununuzi wa Serikali (GPSA) na PSPTB.

**Mheshimiwa Spika,** Taasisi hizo zinatumia mapato yao ya ndani kama matumizi mengineyo (OC) ndio maana hakuna fedha zozote za OC ambazo Taasisi hizi zinapokea kutoka Serikali Kuu. Ni ushauri wa Kamati kuwa kwa kuwa mapato ya Chuo yatokanayo na ada, ni muhimu Serikali ikaweka utaratibu wa kuyatambua mapato haya ili kudhibiti matumizi yasiyo ya lazima.

## 4.3 Usimamizi na utekelezaji wa Sheria ya Bajeti .

**Mheshimiwa Spika**, moja ya lengo la kuanzisha sheria ya Bajeti ilikuwa ni kuwa na Sheria ya mahsusi ya kuongoza mchakato mzima wa bajeti ya Serikali pamoja na kubainisha vema mipaka ya kiutendaji na kimajukumu kati ya Serikali na Bunge kwa kuweka bayana kazi na majukumu ya Serikali na Bunge (pamoja na Kamati zake) katika mchakato wa Bajeti ya Serikali

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na uwepo wa Sheria hii na Sheria nyingine za fedha, bado kuna viashiria vidogo vinavyoonyesha Wizara ya Fedha na Mipango kutozingatia Sheria ya Bajeti katika upangaji na utekelezaji wa Bajeti za mafungu mbalimbali. Mathalani, wakati wa mjadala huu wa Bunge la Bajeti, Serikali kupitia Wizara na Fedha na Mipango ilihamisha kiasi cha takribani **shilingi Bilioni 152** kutoka katika fungu 21 (HAZINA) kwenda TAMISEMI-56 **(Bilioni 33),** Ujenzi-98 **(Bilioni 90**) na Elimu – 46 **(Bilioni 29)** pasipo kushauriana na Kamati ya Bajeti, licha ya kuwa hapo awali Kamati ya Bajeti ilikwishapitisha Bajeti ya mafungu yote ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuzingatia ukomo wa bajeti ambao umekuwa ukisisitizwa na Wizara ya Fedha na Mipango kwa mafungu yote. Kamati inashauri Wizara ya Fedha na Mipango kuhakikisha inasimamia na Sheria ya Bajeti katika kupanga na kutekeleza Bajeti ya Serikali kwa mafungu yote.

## 4.4 Uhakiki na Ulipaji wa Madeni ya Watumishi, Wakandarasi na Wazabuni.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada za kendelea kuhakiki na kulipa madeni ya wafanyakazi, wazabuni na

watoa huduma. Hata hivyo, suala hili limekuwa la muda mrefu na madeni mapya yanaendelea kuzalishwa. Kati ya mwaka 2016/17 hadi Machi 2019 jumla ya **shilingi 2,299,836,402,880.07** zilikuwa zimetolewa kwa ajili ya kulipa madeni mbalimbali ya watumishi, wazabuni, wakandarasi/wahandisi washauri, watoa huduma na madeni mengineyo.

Kuhusu madeni yaliyokataliwa kwa hesabu zilizoishia tarehe 30 Juni 2018 ni jumla ya **shilingi 407,009,218,378.55, Dola za Marekani 29,650,115.78, Euro 162,009, Paundi za Uingereza 7,477**, **Randi za Afrika Kusini 1,122,852 na Korona za Uswis 95,986**. Madeni hayo yalikataliwa kwa sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kukosekana kwa nyaraka zinazostahili.

**Mheshimiwa Spika,** ni rai ya Kamati kuwa Serikali inahakikisha inaendelea na ulipaji wa madeni yote yaliyohakikiwa ili kupunguza gharama kwa Serikali hasa kwa madeni yenye ongezeko la riba lakini pia gharama kwa watoa huduma waliokopa kwenye mabenki kupata mtaji ili waweze kutoa huduma kwa Serikali. Aidha, kwa madai yaliyokataliwa Serikali ihakikishe inawapa taarifa wadai kuhusu mapungufu katika madai yao na hivyo kuwataka wayawasilishe tena yakiwa yamekamilika ili endapo yatastahili kulipwa malipo yaweze kufanyika. Mwisho, muda unaotumika kuhakiki madeni umekuwa mrefu hivyo Serikali ihakikishe kuwa mchakato wa uhakiki unafanyika ndani ya muda ili kuwezesha ulipaji wa mdeni hayo kwa wakati.

### 4.5 Fungu 13 – Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu

**Mheshimiwa Spika**, Kitengo hiki kina jukumu muhimu la kupokea na kuchambua taarifa za miamala shuku toka kwa watoa taarifa na

kupeleka intelligensia kwenye vyombo vya utekelezaji wa Sheria kwa uchunguzi. Pamoja na kwamba kitengo hicho kimeongezewa majukumu lakini Bajeti ya kitengo hicho ni sawa na ile ya mwaka wa fedha wa 2018/19. Katika mwaka wa fedha 2019/20 kitengo kimeidhinishiwa kutumia jumla ya kiasi cha **shilingi 2,015,586,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikiwa sawa na bajeti ya mwaka 2018/19. Kutokana na umuhimu wa chombo hiki, Serikali ikiangalie chombo hiki kwa jicho la kipekee, ihakikishe kuwa kitengo hiki kinatengewa rasilimali fedha za kutosha ili kitekeleze majukumu yake kikamilifu.

### 4.6 Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu Sura ya 423 "The Anti Money Laundring Act Cap 423)

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali iangalie upya sheria Udhibiti wa Fedha Haramu *(The Anti Money Laundering Act cap 423*) na majukumu yake yaangaliwe upya ili iendane na hali halisi ya sasa ili kiweze kufanya zaidi ya kazi iliyokusudiwa. Maboresho hayo yajikite katika maeneo yanayohusu dhamana na kiwango cha fedha ambacho my anaruhusiwa kubeba (cash) hasa kwa wafanyabiashara wa madini baada ya kuanzisha masoko ya madini nchini. Sheria ya *Anti-Money Laundering* ya mwaka 2006 imetaja kiwango cha juu cha fedha ambacho mtu anaweza kukibeba kama fedha taslimu "cash" kuwa ni **shilingi 10,000,000** tu**.** Kiwango hiki kwa biashara ya dhahabu ni kidogo sana, hivyo Sheria iweke utaratibu ambao utawezesha biashara hii kufanyika bila ya kuwa na vikwazo vyovyote.

## 4.7 Uanzishwaji wa Akaunti ya Pamoja ya Fedha

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 133 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania inatamka kuwa kutaanzishwa Akaunti ya Fedha ya Pamoja kwa madhumuni ya shughuli za Jamhuri ya Muungano kwa Mambo ya Muungano ambamo kutawekwa fedha yote itakayochangwa na Serikali mbili kwa kiasi kitakachoamuliwa na Tume ya Fedha ya Pamoja kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Bunge. Aidha, pamoja na Tume hii kuanzishwa mwaka 2003 hadi hivi sasa akaunti hii bado haijafunguliwa.

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa kupitia bajeti ya Fungu hili Kamati ilijulishwa kuwa suala hili linafanyiwa kazi na Serikali ambapo taarifa ya mapendekezo ya mwongozo wa uendeshaji na usimamizi wa Akaunti ya Fedha ya Pamoja (AFP) imewasilishwa Serikalini kwa ajili ya kufanyiwa maamuzi. Hivyo basi, Kamati inashauri Serikali kuharakisha mchakato wa kuandaa Mwongozo kwani suala hili ni la muda mrefu. Uwepo wa akaunti hiyo sio tu utapelekea Tume kufanya kazi iliyokusudiwa lakini pia itasaidia kupunguza kero na changamoto za Muungano.

## 4.8 Uunganishwaji wa Taasisi za Mafunzo zilizo chini ya Wizara mbalimbali

**Mheshimiwa Spika,** Taasisi za mafunzo hasa zile zilizochini ya Wizara mbalimbali mathalani IAA, IFM, Chuo cha Madini, Chuo za Hombolo n.k. zimekuwa zikiongezeka kwa kasi nchini. Pamoja na nia nzuri za uanzishwaji wa Taasisi hizi ambazo zililenga kutoa mafunzo ya kinadharia katika taaluma za Wizara husika taaisi hizi sasa zinatoa hadi shahada. Hivyo basi, imefika wakati sasa wa Serikali ifanye

mapitio ya Sheria zilizoanzisha Taasisi ili kuendana na dhima ya uanzishwaji wa taasisi hizo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa hali ilivyo sasa gharama ya uendeshaji wa vyuo hivi imekuwa kubwa na vimekuwa vikipata ruzuku kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kugharamia mishahara ya Taasisi hizo. Kamati inashauri Serikali kuangalia uwezekano wa kuziunganisha taasisi hizi za mafunzo ili baadhi ziwe makao makuu (Kampasi Kuu) na nyingine kuwa kampasi ndogo. Ama kuziacha Taasisi hizi zijiendeshe kama vyuo vikuu ili kupunguza mzigo wa kibajeti kwa Serikali.

## 4.9 Utitiri wa Mifumo ya Malipo

**Mheshmiwa Spika,** kumekuwa na mifumo mingi sana ambayo inasimamiwa na Wizara mfano TANePS, IFMS, GePG, GSSP, GAMIS, GARI-ITS, IDEA, PMS-Poverty Management System na CBMS. Mifumo yote hii inasimamiwa na Wizara moja na uendeshaji wake ni wa gharama kubwa. Mathalani kwa mwaka wa fedha 2019/20 mifumo hii inakadiriwa kutumia takribani jumla ya **shilingi 3,000,000,000 kila mwaka.** Ni maoni ya Kamati kuwa Serikali ije na namna bora ya kuunganisha mifumo hii hasa ile ambayo Inafanya kazi moja.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia ilibaini kuwa asilimia kubwa ya mifumo hiyo ni ya nje (kununua) na hivyo kuongeza gharama za kiuendeshaji ikiwa ni pamoja na ada za leseni, *hosting* na *subscription fees*.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na changamoto zilizotajwa hapo juu, Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada zake ilizoanza katika

kuhakikisha kuwa inakuja na mifumo yake yenyewe ambapo hadi sasa imeweza kutengeza mifumo yake kadhaa ikiwa ni pamoja na mfumo wa PMIS, TANePS, GePG, EFD na GAMIS. Hivyo basi, Serikali iharakishe mchakato wa kujenga mifumo yake na kuondokana na mifumo mengine kutoka kwa Makampuni au watu binafsi.

### 4.10 Utekelezaji wa Akaunti Jumuifu ya Fedha (TSA)

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na dhamira nzuri ya Serikali ya kuhuisha akaunti zote za Serikali na kuanzisha Akaunti Jumuifu ili kudhibiti matumizi, mfumo huu umekumbwa na changamoto mbalimbali za kiutendaji. Mfumo huu kwa kiasi kikubwa unategemea ubora wa mifumo ya mawasiliano na kwa hali ilivyosasa hasa katika ngazi za Halmashauri kumekuwa na changamoto kubwa sana. Tatizo hili la kimtandao limepelekea ucheleweshawaji wa malipo kutokana na kuwa taarifa za malipo hazifiki Benki Kuu kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** changamoto nyingine inayopelekea ufanisi wa mfumo huu kupungua ni mlundikano wa "server" katika kituo kimoja. *Server* zote za malipo zimehifadhia katika ofisi za TAMISEMI makao makuu Dodoma na hivyo kupelekea kituo hiki kuelemewa au kushindwa kufanya kazi iwapo kutatokea hitilafu ya umeme au kimtandao. Ili kuondokana na adha hii na mfumo uweze kufanya kazi kwa ufanisi na kwa matarajio yaliyokusudiwa ni vema Serikali ikatatua tatizo hili la kimtandao na kulipatia ufumbuzi wa kudumu ikiwa ni pamoja na kuzitaka taasisi, idara na wizara zote kuonganishwa katika mkongo wa Taifa. Aidha, Serikali ione umuhimu wa wa kuanzisha kituo cha *server* kwenye kila kanda ambapo kuna ofisi za Benki Kuu kwa lengo la kupunguza mzigo uliopo Ofisi ya Rais – TAMISEMI kuongeza ufanisi.

## 4.11 Fedha kwa ajili ya Ujenzi wa Maboma

**Mheshimiwa Spika,** katika kuunga mkono juhudi za wananchi za ujenzi wa miundombinu ya mandeleo, Kamati ilikubaliana na Serikali kuhusu suala la kumalizia maboma na ikatenga kiasi cha **shilingi bilioni 271.33**. Aidha Serikali ilikubali kupeleka fedha hizo katika Halmashauri kwa awamu, ambapo hadi mwezi Januari ilipeleka kiasi cha **shilingi bilioni 29.9** kwa ajili ya miradi ya elimu **na shilingi bilioni 38.9** kwa miradi ya afya**.** Shilingi **54.75** zilitolewa kupitia mradi wa Lipa Kulingana na Matokeo kwa ajili ya kumalizia miradi ya elimu. Aidha, miradi ya afya imeendelea kutengewa fedha kwa kuzingatia tathmini ya mahitaji ambapo jumla ya **shilingi bilioni 100.5** zilmetolewa kwa mwaka 2018/19. Kamati inaendelea kusisitiza upelekaji wa fedha zilizobaki katika mwaka wa fedha 2019/20 kwa ajili ya kuendelea na ukamilishaji wa maboma 144 ya miradi ya afya na elimu.

## 4.12 Taasisi zinazosimamia manunuzi ya Umma

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata fursa ya kupitia bajeti pamoja na utendaji wa mashirka yaliyo chini ya Wizara hii. Kati ya mashirika ilikutana nayo ni pamoja na taasisi zinazohusiana na masuala ya ununuzi wa umma zikiwemo GPSA – Wakala wa Hudma ya Ununuzi Serikalini, PPRA – Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma, PSPTB – Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi Tanzania na PPAA – Mamlaka ya Rufaa ya Zabuni za Umma.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwepo na mwingiliano wa majukumu baina ya hizi taasisi kwani baadhi ya taasisi hizi zinafanya kazi zinazofanana. Hivyo Kamati inashauri kuwa

kuwepo na kutafsiri majukumu kwa uwazi baina ya taasisi hizi. Taasisi zihakikishe kuwa zinatekeleza majukumu yake kama yalivyoanishwa kwenye Sheria ilizozianzisha. Aidha, Kamati ilibaini kuwepo na changamoto ya wataalam wa ununuzi waliosajiliwa na bodi ya PSPTB kwenye taasisi na mashirika ya Serikali na hivyo kwenda kinyume na Sheria suala ambalo ni lazima Serikali ilifanyie kazi kwa haraka.

### 4.13 Usiamamizi wa Maduka ya Ubadilishaji Fedha (bureau de change)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada zake katika kusimamia biashara ya ubadilishaji wa fedha nchini. Hatua hii itaendelea kuimarisha ulinzi na usalama na kukabiliana na mianya yote ya ubadilishaji wa fedha haramu. Hata hivyo, endapo Serikali haitaimarisha mifumo yake itatoa mianya ya kuwepo kwa maduka ya ubadilishaji fedha yasiyo rasmi "*black market*".

**Mheshimiwa Spika,** Ni vema Serikali ikaangalia viwango vya ubadilishaji fedha vinavyotolewa na mabenki kwani ni vya juu ukilinganisha na vile vinavyotumika na maduka ya ubadilishaji fedha. Hivyo basi, Serikali iangalie ni kwa namna gani itaweza kudhibiti viwango vya fedha vinavyotolewa na mabenki, viwango ambavyo vilitegemea kuwa vya chini vikilinganishwa na vya *bureau de change* ikizingatiwa kuwa mabenki yanafanya shughuli nyingine Zaidi ya kubadilisha fdha za kigeni.

## 4.14 Sheria ya Sekta Ndogo ya Fedha ya 2018 (The Microfinance Act 2018).

**Mheshimiwa Spika,** Novemba 2018, Serikali ilileta Muswada wa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha (The Microfinance Act 2018) uliokuwa na madhumuni ya kuwezesha usimamizi na udhibiti wa huduma ndogo za kifedha na Bunge lako tukufu lilipitisha Muswada huo na kuwa Sheria. Pamoja na nia njema ya Serikali ya kusimamia na kudhibiti Sekta ndogo ya fedha nchini ikiwa ni pamoja na kuwatambua wananchi na wafanya biashara nchini walioko katika sekta hiyo kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wadau wanaoitekeleza Sheria hii.

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa Sheria hii umekuwa mgumu kutokana na masharti yaliyowekwa katika Sheria yanayolenga kundi la Tier 4. Masharti hayo ni pamoja na matumizi ya benki katika ukusanyaji na uhifadhi wa fedha za wanakikundi; matumizi ya *credit bureau reference* pamoja na ulazima wa kikundi kuwa na mtaalam wa fedha yaani mhasibu. Masharti hayo yamekuwa vikwanzo kwa Tier 4 na hivyo kushindwa kutekeleza sheria.

## 4.15 Ugharamiaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** Sheria ya Misaada, Mikopo na Dhamana inaipa mamlaka Wizara ya Fedha na Mipango kuchambua na kuishauri Serikali kuhusu fedha za ugharamiaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Kwa msingi huo, Kamati inashauri Serikali badala ya kutumia fedha za ndani katika ujenzi wa miradi ya maendeleo ambayo ina muelekeo wa kibiashara ione umuhimu wa kutafuta fedha nje kupitia mikopo yenye masharti nafuu au kutekeleza miradi

hiyo kwa kwa njia ya ubia. Hatua hii itasaidia fedha za ndani kuelekezwa kwenye miradi ya kijamii.

### 4.16 Mwenendo wa Utolewaji wa Fedha za Bajeti kwa Mafungu ya Wizara

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaisistizia Wizara kuhakikisha kuwa fedha za bajeti kwa ajili ya mafungu yake zinatolewa kama zilivyoidhinishwa na Bunge. Kamati inashauri kuwa wakati wa uandaaji wa bajeti hasa bajeti ya maendeleo Wizara isitenge kiasi kikubwa cha fedha kwa kutegemea fedha za wafadhili kutoka nje, kwani mwenendo wa upokeaji fedha za maendeleo za nje sio wa kuridhisha na hivyo kukwamisha utekelezaji wa bajeti na shughuli za Wizara.

### 4.17 Ukusanyaji wa Mapato ya Kodi na yasio ya Kodi

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha miaka mitatu, Mamlaka ya mapato Tanzania imekuwa ikikusanya kwa wastani kati ya **shilingi 1,2000,000,000,000** hadi **1,300,000,000,000** kwa mwezi. Hatua hii ni ya kupongeza kwasababu kabla ya hapo Mamlaka ilikuwa ikikusanya wastani wa **bilioni 800,000,000,000** hadi **shilingi 900,000,000,000** kwa mwezi.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na pongezi hizo, Kamati inaishauri Serikali na Mamlaka ya Mapato Tanzania mambo yafuatayo; kwanza kupanua wigo wa kodi na pili ni kuhakikisha kwamba Maofisa wa TRA pindi wanapokuwa wanatekelezeja majukumu yao kuzingatia sheria, taratibu na kanuni.

## 4.18 Mapungufu ya usimamizi wa Sera za Kibajeti na Kifedha (Fiscal and Monetary Policies

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua jukumu la Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na taasisi zake katika kusimamia Sera za Kibajeti na Fedha (Fiscal and Monetary Policies) ili kuleta uchumi tulivu na hivyo kusaidia ukuaji wa uchumi (*economic growth*) unaoendana na maendeleo ya uchumi (*economic development*). Aidha, pamoja na makujukumu haya, Wizara ya Fedha na taasisi zake zimekuwa zikichukua baadhi ya hatua za kisheria, kikanuni pamoja na za kiutawala (*administrative measures*) katika kusimamia shughuli za kiuchumi. Hata hivyo, mapungufu katika utekelezaji wa baadhi ya hatua hizo umekuwa ukiathiri uendeshaji wa shughuli za kibiashara na hivyo kudhoofisha kasi ya uwekezaji katika sekta mbalimbali, mathalani utozaji wa 15% ya amana kwa waagizaji wa sukari ya viwandani, usitishwaji wa kutoa huduma ya kubadilishia fedha kwa baadhi ya maduka, na kuchelewa kurudishwa kwa rejesho la Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT refunds). Kamati inaishauri Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na taasisi zake kuhakikisha inazingatia sheria, kanuni na taratibu ilizojiwekea katika kusimamia sera za kibajeti na fedha katika kuhakikisha zinasaidia kuweka mazingira wezeshi ya ufanyaji biashara nchini pamoja na uwekezaji na hivyo kusaidia ukuaji wa uchumi .

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** naomba nihitimishe kwa kukushukuru wewe Mhe. Spika, Dkt. Tulia Akson, Mb - Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa miongozo yenu ambayo mmekuwa mkitupatia. Shukrani pia ziwaendee Mhe. Dkt Philip Mpango (Mb) Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Dkt Ashatu K. Kijaji (Mb), Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Katibu Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu pamoja na wataalamu wote wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao mkubwa waliotupa wakati wote wa kujadili utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Aidha, Kamati inatoa shukrani kwa Wakuu wa Taasisi na Idara zote zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa ushirikiano na ufafanuzi walioutoa kwa Kamati katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee kabisa napenda kumshukuru Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi Makamu Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Wajumbe wote wa Kamati kwa umahiri, umakini na ushirikiano wao walionipatia wakati wote wa kuchambua bajeti ya Wizara hii na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Aidha, naomba niwatambue Wajumbe wa Kamati kwa majina yao kama ifuatavyo: -

1. Mhe. George Boniface Simbachawene, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb - Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajabu, Mb
4. Mhe. Ali Hassan Omar, Mb
5. Mhe. Abdallah Majura Bulembo, Mb
6. Mhe. Prof. Anna Kajumulo Tibaijuka, Mb
7. Mhe. Albert Obama Ntabaliba, Mb
8. Mhe. Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mb

9. Mhe. David Ernest Silinde, Mb
10. Mhe. Freeman Aikael Mbowe, Mb
11. Mhe. Hasna Sudi Katunda Mwilima, Mb
12. Mhe. Dkt. Immaculate Sware Semesi, Mb
13. Mhe.Dkt. Balozi Diodorus Buberwa Kamala, Mb
14. Mhe. Makame Kassim Makame, Mb
15. Mhe. Maria Ndilla Kangoye, Mb
16. Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb
17. Mhe. Mendrad Lutengano Kigola, Mb
18. Mhe. Marwa Ryoba Chacha, Mb
19. Mhe. Mbaraka Kitwana Dau, Mb
20. Mhe. Oran Manase Njeza, Mb
21. Mhe. Riziki Said Lulida, Mb
22. Mhe. Stephen Julius Masele, Mb
23. Mhe. Andrew John Chenge, Mb
24. Mhe. Hussein M. Bashe, Mb
25. Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb
26. Mhe. Suleiman A. Sadiq, Mb
27. Mhe. Jumanne Kishimba, Mb.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Katibu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagaigai pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha, kwa namna ya pekee napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti kwa kuratibu shughuli za Kamati pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na mafungu manane (8) yaliyo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

George B. Simbachawene (Mb)
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI**

03 Juni, 2019